

Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 1 hadi 5

Musa : Sabalkheri Kito?

Kito : Aheri Musa. Habari ya likizo?

Musa : Njema kabisa. Labda yako. Ulitekeleza shughuli ipi wakati wa likizo?

Kito : Nilimtembelea nyanyangu. Nilimsaidia kufanya shughuli mbalimbali za nyumbani na shambani. Nilikuwa na wakati mzuri mno.

Musa : (Akitabasamu) Si ulifurahia ngano za nyanya?

Kito : Bila shaka. Kwanza hadithi ya "Sungura na Fisi" ilinifurahisha mno.

Musa : (Akitikisa kichwa) Hata mimi nitamtembelea nyanyangu likizo ijayo.

Kito : Hakika msena wangu. Basi tuketi tujiandae kwa masomo.

Musa : Ahsante kwa wakati wako. (Wote wanaketi)

- | | |
|--|---|
| 1. Musa alimsalimia Kito "Sabalkheri", Je ulikuwa wakati upi?
A. Jioni
B. Mchana
C. Asubuhi
D. Usiku | B. kufanya kazi za nyumbani
C. kuvatembelea marafiki zetu
D. kuzurura sokoni |
| 2. Ni nini kinachoonyesha kuwa Musa ana heshima na adabu?
A. Anaanza kwa kumsalimia Kito
B. Anamuuliza Kito maswali mengi
C. Anaahidi kumtembelea nyanyake
D. Alifurahia sana kuzungumza na Kito | 4. Kito alifurahia nini alipokuwa kwa nyanyake?
A. Chakula cha nyanya
B. Hadithi za nyanya
C. Safari za mbali
D. Kufanya maombi |
| 3. Kulingana na mazungumzo haya, tunaweza kuwasaidia wazazi wetu kwa njia ipi nyumbani?
A. kucheza mchana kutwa | 5. Neno lingine lenye maana sawa na "msena" ni
A. adui
B. mpwa
C. somo
D. rafiki |



Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 6 - 10

Afya ni hali ya kujisikia vizuri kimwili, kiakili, kiroho na kiotu bila kusumbuliwa na ugonjwa wowote. Afya ya binadamu itakuwa njema kama atafuatilia kanuni na taratibu bora za afya. Hiyo inajumlisha mlo kamili, yaani chakula chenye viruyubishi vyote, vikiwemo protini, wanga na mafuta, japo kwa kiasi na vitamini. Pia, anatakiwa awe safi mwilini na mazingira yake, kama vile kwa kuoga na kusafisha mazingira yake. Mandhari yenye hewa safi pia husaidia katika kuhifadhi afya ya binadamu katika mwili na akili.

Mazingira mara nyingi huchukuliwa kuwa jambo muhimu katika afya ya binadamu. Hii inajumuisha mazingira ya asili, mazingira ya kujengwa na mazingira ya kijamii. Pia, mambo kama vile maji safi na hewa, makazi salama, huchangia afya njema, hasa kwa watoto. Aidha, mja anatakiwa kuwa na afya ya kiroho, yaani kuishi kadiri ya mafundisho ya mwenyezi Mungu kama vile kupendana na wengine, kuthaminiana na kuacha dhambi.

6. Hali ya kujisikia vizuri kimwili, kiakili, kiroho na kiutu huitwa?
 A. afya B. kunenepa
 C. usawa D. utajiri
7. Afya ya binadamu itakuwa njema ivapo;
 A. atakuwa na pesa nyingi
 B. atafuatilia kanuni bora za afya
 C. atakuwa na marafiki wengi
 D. atakula chakuka kingi
8. Vifuatavyo ni virutubishi vinavyopatikana katika vyakula ila;
 A. Wanga B. Protini
 C. Wadudu D. Vitamini
9. Afya njema hujumlisha mambo haya yote ila;
 A. Kula vyakula bora
 B. Usafi wa mwili
 C. Usafi wa mazingira
 D. Mavazi machafu
10. Neno "mlo" katika kifungu linamaanisha?
 A. afya B. chakula
 C. usafi D. maradhi



Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 11 - 15

Mapambo ni vitu vinavyovaliwa mwilini ili kumfanya mtu awe wa kuvutia. Kuna aina mbalimbali ya mapambo. Aidha, kuna mapambo ya kike na ya kiume. Kwa mfano, ushanga ni pambo la kike linalovaliwa shingoni. Mapete, kipuli na bali vile nayo huvaliwa masikioni. Nyerere au furungu huvaliwa miguuni ilhali hina hupakwa kwenye sehemu mbalimbali za mwili kama vile mikono na miguu. Ni vizuri kuyatumia mapambo vizuri na kuyavaa sehemu yafaayo.

11. Mapambo ni nini?
 A. Vitu vinavyouzwa bei ghali
 B. Vitu vya kuvutia vinavyovaliwa mwilini
 C. Vitu vyovyote vya dhamani
 D. Vitu ambavyo humetameta
12. Bali na ushanga, taja pamba jingine linalovaliwa shingoni.
 A. kidani B. kishaufu
 C. chale D. kipuli
13. Chagua mapambo yanayovaliwa masikioni kati ya haya.
 A. Ushanga, kikuba, furungu
 B. Herini, pini, taji
 C. Mkanda, kikero, kishaufu
 D. Mapete, kipuli, bali
14. Nyerere huvaliwa wapi?
 A. mkononi
 B. kiunoni
 C. miguuni
 D. nyweleni
15. Mwandishi anatoa ushauri gani?
 A. Tuvavalie mapambo sehemu yoyote
 B. Tuvatumie mapambo vizuri
 C. Tuvavalie mapambo mengi
 D. Tusivavale mapambo yoyote

Soma kifungu kifuatacho . Kwa kila swali 16 hadi 20, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa

Kila siku _____ 16 _____ kutoka shuleni, Kazungu hufanya mazoezi. _____ 17 _____ hucheza kwa kutumia mpira _____ 18 _____. Aidha, hufanya mazoezi ya kukimbia _____ 19 _____ kunyosha viungo vya mwili. Anajua kuwa kufanya mazoezi ni jambo _____ 20 _____.

- | | | | |
|-----------------|----------------|------------|-------------|
| 16. A. kabla ya | B. badala ya | C. kati ya | D. baada ya |
| 17. A. Wewe | B. Yeye | C. Wao | D. Nyinyi |
| 18. A. yake | B. lake | C. wake | D. zake |
| 19. A. ili | B. k wa sababu | C. kama | D. lakini |
| 20. A. mzuri | B. kizuri | C. lizuri | D. nzuri |

Tumia neno sahihi kwenye mabano kujaza pengo

21. Kitabu _____ ni cha mtoto huyu.
A. hiki B. kiki
C. hii D. hilo
22. Nyumba _____ ni yao.
A. yule B. kile
C. lile D. ile
23. Viti _____ vitatumiwa na wageni.
A. hizo B. hio
C. hivyo D. hiyo

Kamilisha sentensi kwa kiulizi sahihi

24. Ni vitabu _____ vilivyopotea?
A. ipi B. vipi
C. lipi D. yupi
25. Tunda _____ limeiva?
A. kipi B. lipi
C. ipi D. vipi
26. Chumba _____ kilichojengwa?
A. nani B. kigani
C. zipi D. gani

Chagua jibu sahihi swali la 27 hadi 30

27. Tumia "amba" kujaza pengo.
Chakula _____ kimepikwa ni kitamu.
A. ambao B. ambayo
C. ambacho D. ambalo
28. **Chagua kivumishi cha sifa sentensi ifuatayo.**
Mwalimu mzuri alitupa zawadi.
A. mzuri B. mwalimu
C. zawadi D. alitupa
29. **Kanusha sentensi ifuatayo:**
Wakulima watapanda mwakani.
A. Wakulima hawapandi mwakani.
B. Wakulima hawatapanda mwakani.
C. Wakulima hawakupanda mwakani.
D. Wakulima hawangepanda mwakani.
30. **Kamilisha methali hii**
Asiyesikia la mkuu _____
A. huona shida
B. hana aambiwalo
C. hujaa hila
D. huvunjika guu